



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI GEITA



Kumb. Na. KB. 394/586/01 'A'/72

Tarehe:11/01/2023

**YAH: TANGAZO LA KAZI ZA URASIMISHAJI WA MAKAZI YASİYOPANGWA
KATIKA HALIMASHAURI YA MJI WA GEITA**

1. UTANGULIZI

Halmashauri ya Mji Geita ilianzishwa na kutangazwa rasmi katika gazeti la Serikali mwaka 2012. Halmashauri hii ni kitovu cha shughuli nyingi za kiutawala, kijamii na kiuchumi katika Mkoa wa Geita. Hali hii imesababisha ukuaji wa haraka wa idadi ya watu na uchumi katika Mji wa Geita na Mkoa kwa ujumla. Mji wa Geita ni kati ya miji nchini inayojengeka na kukua kwa haraka sana hata maeneo ambayo hayajapangwa.

2. MITAA YA URASIMISHAJI

Ili kuboresha makazi ambayo hayajapangwa, Halmashauri inatangaza nafasi kwa makampuni ya upangaji na upimaji kuomba kazi za urasimishaji kwa mitaa 19 ambayo ina sifa za kurasimishwa. Mitaa hiyo ni **Mwatulole (Nguzombili, Kishimbenzobe na Fadhili bucha) Nyantorotoro A, Buchundwankende, Nyamakale, Mgusu, Machinjioni, Katoma, Compaundi, Mbugani, Mpomvu, Majengo, Mkangala, Kanyala, NMC, Nyampa, Kigoma road, Kasamwa, Mwembeni na Nshinde** kama ilivyooneshwa katika jedwali hapo chini.

11 Barabara ya Geita TC, Mtaa wa Magogo. S.L.P 384, 30182 GEITA. Simu 0282520437, Nukushi 0282520437. Barua pepe : td@geitac.go.tz, Tovuti : www.geitac.go.tz

Makadrio ya viwanja vitakavyorasimishwa

NA.	MTAA	IDADI YA VIWANJA TEGEMEW A	NA.	MTAA	IDADI YA VIWANJA TEGEMEWA
1	Mwatulole	3500	11	Majengo	2000
2	Compaund	1000	12	Mkangala	1800
3	Nyantorotoro A,	2200	13	Kanyala,	2000
4	Buchundwanken de,	1800	14	NMC,	1500
5	Nyamakale,	1800	15	Nyampa,	1500
6	Mgusu,	1500	16	Kigoma road	2000
7	Machinjioni,	1800	17	Kasamwa,	1800
8	Katoma,	1500	18	Mwembeni	1300
9	Mpomvu	1500	19	Nshinde	1500
10	Mbugani	600			
JUMLA		17,200	JUMLA		15,400
	JUMLA KUU			32,600	

11 Barabara ya Geita TC, Mtaa wa Magogo. S.L.P 384, 30182 GEITA. Simu 0282520437, Nukushi 0282520437. Barua pepe : td@geitadc.go.tz, Tovuti : www.geitadc.go.tz

3. SIFA ZINAZOTAKIWA

- i. Kampuni inatakiwa kuwa na mtaji wa kuanzia kazi usiopungua robo ya gharama za mradi kwa mtaa unatakaopewa.
- ii. Kama inavyoelekezwa katika mwongozo wa urasimishaji makazi yasiyopangwa nchini wa mwaka 2021 ni lazima kampuni ya upangaji inayoomba kazi lazima iwe na makubaliano na kampuni ya upimaji, hivyo kampuni ya upimaji inayoomba kazi lazima iwe na makubaliano na kampuni ya upangaji.
- iii. Kampuni lazima iwe imesajiliwa na bodi ya kitaaluma yaani Bodi ya Usajili ya Wataalam wa Mipango Miji kama kampuni ni ya upangaji au Halmashauri ya Wapima Ardhi Tanzania kama kampuni ni ya upimaji
- iv. Kampuni lazima iwe na cheti cha usajili kutoka BRELA
- v. Kampuni lazima iwe na ofisi yenye anwani kamili ya mahali ilipo
- vi. Iwe na leseni hai inayoiruhusu kufanya kazi za Mipangomiji au upimaji nchini;
- vii. Iwe na wataalamu wa kutosha na wenye ujuzi na uwezo sahihi wa fani ya Mipangomiji waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango miji au Halmashauri ya Wapima Ardhi Tanzania watakaofanya kazi za ushauri na za uwandani
- viii. Iwe haidaiwi kodi yoyote na Serikali; na
- ix. Isiwe na mgongano wa maslahi.
- x. Kampuni iwe na uwezo wa kumaliza mtaa mmoja ndani ya muda wa miezi mitatu tangu kupewa kazi katika mtaa huo.

4. JINSI YA KUOMBA

Kampuni binafsi au taasisi iliyo na sifa tajwa hapo juu inakaribishwa kutuma maombi kabla au siku ya tarehe **25/01/2023** kwa Mkurugenzi wa Mji **S.L.P 384 GEITA** kwa barua ya maombi iliyosainiwa na mkurugenzi mkuu wa kampuni ikiwa imeambatanishwa na Uzoefu wa kazi za urasimishaji (company profile), Leseni hai vyeti vya usajili wa BRELA na bodi za kitaaluma.

Tangazo hili limetolewa na;



Egidy Teulas

Kaimu Mkurugenzi wa Mji

GEITA
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
GEITA

Nakala:- Mbao za Matangazo na katika Tovuti ya Halmashauri.